**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

*Simu: +255262963309/13/14*
*Nukushi: +255 262 963 316*
*Barua pepe: ps@lands.go.tz*
*Tovuti: www.lands.go.tz*

*Mji wa Serikali, Mtumba,*
*S. L. P. 2908,*
***40477* DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU UVUNJWAJI WA MAKAZI YA WANANCHI WALIOJENGA KWENYE SHAMBA NA. 26 LENYE UKUBWA WA EKARI 6,385.2 LILILOPO KATIKA KIJIJI CHA GEZAULOLE KATA YA MAKURUNGE WILAYA YA BAGAMOYO

**31 Julai 2026 Dodoma**
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia vyombo mbalimbali vya Habari imepokea taarifa kuhusu uvunjwaji wa maendelezo ya wananchi takribani 110 wa Kijiji cha Gezaulole Kata ya Makurunge Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani. Taarifa zinaonesha zoezi hilo limetekelezwa na kampuni ya Nolic Company Ltd ambayo ni Dalali wa Mahakama.

Uvunjwaji huo umefanyika katika shamba namba 26 Makurunge kutokana na utekelezaji wa maamuzi ya Mahakama Kuu katika **Shauri la Madai ya Ardhi Na.19896 la mwaka 2024**. Katika Shauri hilo, wamiliki wa shamba kwa **Hati Milki Na. 36911**, **Kampuni ya Azania Agricultrural Enterprises Limited** walifungua madai dhidi ya wananchi waliofanya maendelezo katika shamba hilo. Wananchi hao walishindwa katika shauri hilo na iliamuriwa waondolewe kwa utaratibu wa kimahakama.

Kwa mujibu wa **Ibara ya 4** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama ndio chombo cha kutafsiri sheria na kutoa haki. Vilevile, kwa mujibu wa **Ibara ya 107A** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mamlaka yenye uamuzi wa mwisho wa utoaji haki ni Mahakama.

Hivyo, Wizara pamoja na mamlaka nyingine za Serikali ziliheshimu maamuzi hayo na kwa hali hiyo, upande ambao haujaridhika na maamuzi hayo, utapaswa kukata rufaa dhidi ya maamuzi husika kupitia mhimili wa Mahakama.

Wizara imeendelea kwa nyakati tofauti, kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utaratibu wa kupata ardhi nchini kwa njia halali ambao ni kwa kununua, kurithi au kupewa kutoka kwa

mmiliki husika. Kutofuata taratibu hizi kumesababisha athari kubwa kwa wananchi ambao huingia katika migogoro na wamiliki wa maeneo husika, uharibifu wa mali na madhara mengine mengi.

Kufuatia hatua hiyo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt. Leonard Akwilapo ametoa wito kwa wananchi wote kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kupata ardhi ili kuepuka migogoro inayotokana na madai ya umiliki wa ardhi. Aidha, amesisitiza kuwa wananchi wanapaswa kutumia Ofisi za Ardhi kwenye Halmashauri na Mikoa kuhakiki maeneo wanayoyahitaji kabla ya kufanya uendelezaji.

Vilevile amewaagiza watendaji wote wa Sekta ya Ardhi kuhakikisha wanakagua maeneo yote yasiyoendelezwa na kuchukua hatua dhidi ya wamiliki hao kwa kuzingatia Sheria.

Imetolewa na



Eleuteri Mangi

**MKURUGENZI KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**